**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

Shule ya Sekondari Kisimiri,

S.L.P 14480,

**ARUSHA**

Kumb. Na. KSS/CG/VOL.111/19 21/05/2021

Ndg MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI............................................................

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISIMIRI ILIYOKO KATIKA HALMASHAURI YA MERU MKOA WA ARUSHA MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao **amechaguliwa kujiunga na** Kidato cha Tano mwaka **2021** tahasusi ya **........................** Shule ya Sekondari Kisimiri iliyopo umbali wa kilometa **65** kutoka mjini Arusha. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi Arusha mjini magari ya kuelekea Ngarenanyuki na yanayofika Kisimiri, kupitia hifadhi ya Taifa ya Arusha nauli ni shilingi elfu nne **(4,000)** tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **05/07/2021**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe**05/07/2021**. Masomo yataanza rasmi tarehe ya kufungua shule.

## A. MAAGIZO YA FEDHA

Mchanganuo wa malipo ni kama unavyoonekana hapa chini:

| MAELEZO | KIASI | MUDA |
|---|---|---|
| Ada | Tsh 70,000/=<br>Tsh 35,000/= kila mhula | Kwa mwaka |
| Ulinzi, ukarani na upishi | Tsh 30.000/= | Kwa mwaka |
| Ukarabati | Tsh 15,000/= | Kwa mwaka |
| Taaluma | Tsh 20,000/= | Kwa mwaka |
| Picha, Kitambulisho na Nembo | Tsh 13,000/= | Mara moja |
| Matibabu na huduma ya kwanza | Tsh 10,000/= | Kwa mwaka |
| Tahadhari (haitarejeshwa) | Tsh 5,000/= | Kwa mwaka |
| Mahafali | Tsh 5,000/= | Kwa mwaka |
| Mitihani ya Upimaji (Mock) | Tsh 20,000/= | Mara moja |
| Jumla ya gharama kwa mwaka | **Tsh 188,000/=** | |

Fedha ya ada na michango mingine iwekwe kwenye akaunti Namba **40801607934** iliyoko Benki ya **NMB.** Jina la akauni hiyo ni **Kisimiri Secondry School. FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA SHULENI.** Mwanafunzi aje na **<u>Nakala halisi ya hati za malipo (Original Bank Pay in Slip).</u>**

## B. MAAGIZO YA MAHITAJI MENGINE

### B.1 SARE YA SHULE

### A) WAVULANA

i. Aje na suruali mbili za rangi ya Blue Bahari zenye marinda mawili tu, kitambaa cha **esteem namba moja** ziwe na mfuko mmoja tu nyuma upande wa kulia, upana chini ya miguu iwe inchi 18 na iwe na turnup (kwa vyovyote vile isiwe modo)

ii. Aje na mashati mawili meupe ya mikono mirefu mapya. Mashati hayo yatapigwa nembo ya shule hapa shuleni

iii. Aje Sweta "V – Shape" Shingoni rangi ya Blue Bahari

iv. Aje na Tai mbili za rangi ya Blue Bahari (ndefu)

v. Aje na suruali mbili (Shamba dress) za zangi ya Kahawia (Mashono ni kama ilivyo kwa sare)

vi. Aje na T- shirt mbili rangi ya Darkblue, shingo ya mviringo

vii. Aje na mikanda miwili ya rangi mweusi ya ngozi wa kufungia suruali

viii. Aje na viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vya ngozi vyenye visigino vifupi

vix. Aje na soksi nyeusi jozi mbili au zaidi

### B. WASICHANA

i. Aje na sketi mbili za rangi ya Blue Bahari zenye drafti kitambaa cha **esteem,** upana wa marinda uwe kati ya Inchi 1 na 2 zenye mikanda (belt) ndogo. Urefu wa chini iwe sentimeta 10 kutoka kwenye unyayo wa miguu (kwa vyovyote vile isiwe fupi)

ii. Aje na mashati mawili meupe ya mikono mirefu mapya. Mashati hayo yatapigwa nembo ya shule hapa shuleni

iii. Aje na Sweta mbili "V – Shape" Shingoni rangi ya Blue Bahari

iv. Aje na sketi jozi mbili za nguo za kazi (Shamba dress) yangi ya Kahawia (Urefu ni kama wa sare)

v. Aje na T- shirt mbili rangi ya Darkblue, shingo ya mviringo

vi. Aje na Tai mbili za rangi ya Blue Bahari (ndefu)

vii. Aje na viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vya ngozi vyenye visigino vifupi

viii. Aje na soksi nyeupe jozi mbili au zaidi

vix. Wanafunzi wa kislamu waje na jozi mbili nyeupe za kijuba (hijab)

**B.2 MAHITAJI NA VIFAA VYA DARASANI**

**a).** Aje na nakala ya **Cheti cha Kuzaliwa** na **Result Slip** ya kidato cha nne

**b**). Madaftari makubwa (counter books yasiyopungua **saba**)

**c).** Alete Rimu moja ya karatasi aina ya Rotatrim

**d).** Kalamu za wino za kuandikia na penseli za kuchorea za kutosha**.**

**e).** Mkoba imara wa kuhifadhia madaftari na vitabu

**B.3 VIFAA VYA USAFI**

a). Jembe moja lililonolewa na mpini wake au Rato na mpini wake

b). Fyekeo lililonolewa/Reki ya mpini wa chuma (Kimojawapo).

c). Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko, na mopa moja kwa wote

d). Ufagio wa ukili kwa wasichana na ufagio wa chelewa kwa wavulana

**C. MAHITAJI YA BWENI**

**i**. Shuka za kulalia mbili light blue kwa wasichana na pink kwa wavulana

**ii.** Blanketi la kawaida (student size 1), Mto, foronya mbili na taulo

**iii**. Godoro imara la futi mbili na nusu kwa sita.

**iv**. Tochi moja kwa ajili ya dharura mwanga unapokosekana.

**v**. Aje na Bukta 2 za rangi ya mayai/njano au nyekundu na T- shirt
zake pamoja na raba za michezo na soksi ndefu za rangi ya kijani au nyekundu.

vi. Aje na Sahani, Bakuli, Kikombe (rangi nyeusi) na Kijiko (Kimoja kimoja)

## D. SHERIA ZA SHULE

Pamoja na barua hii nimeambatanisha makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule moja kwa moja (**Tazama kiambatisho A :**)

## E. MAAGIZO KWA WAZAZI

Sheria mama za shule zimebainishwa katika **kiambatisho A:** Pamoja na fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni za shule zilizotajwa hapo juu na zitakazotolewa na Uongozi wa Shule. Wazazi na mwanafunzi/wanafunzi ni muhimu kusoma kwa uangalifu na kutia saini zenu sehemu ya makubalianano katika **kiambatisho A:** pamoja na **kiambatisho B:** halafu mzirudishe kwa Mkuu wa Shule. Ni dhahiri kuwa wanafunzi watakuwa wanapoteza wakati wao bure kama wasipotaka kufanya kazi zote kwa bidii na kutii Sheria za Shule.

## F. FOMU YA UCHUNGUZI WA KIAFYA

Hakikisha mwanao amepimwa na daktari na kujaza ripoti kwenye "Medical Examination Form" **kiambatisho C:** na irudishwe kwa Mkuu wa Shule siku ya kuripoti shuleni.

## G. TAARIFA ZA MAENDELEO YA MWANAFUNZI

Kila mara mzazi anapelekewa kimaandishi taarifa ya maendeleo ya mwanae katika masomo, kazi na tabia kupitia tovuti yetu **www.kisimirisecondary.com** Ni muhimu mzazi/mlezi usome taarifa hiyo na kuwasiliana na shule kama kuna agizo lolote. Tafadhali wazazi someni taarifa hizo na **KUZINGATIA YALIYOANDIKWA KISHA UWASILIANE NASI KWA NAMBA ZA SIMU ZILIZOPO KWENYE TOVUTI YETU**

## H. HITIMISHO

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto wetu waendelee na wapate kile walichokifuata hapa Shuleni KISIMIRI, yaani ELIMU. Msisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha alama **60%** au zaidi katika kila somo. Sheri zote za shule zinalenga katika kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake. **TUNATEGEMEA SANA USHIRIKIANO WENU**

**KARIBUNI SANA**

**……………………………..**
**TARIMO, VALENTINE M.**
**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATISHO A:**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI KISIMIRI**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Mwanafunzi anayejiunga katika shule hii anapaswa kuzisoma vizuri sheria na kanuni za shule kisha atasaini pamoja na mzazi au mlezi wake wakati wa kuripoti na atarudisha hati hii shuleni.

Mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuishi na kutenda kulingana na maadili ya uanafunzi.
2. Heshima miongoni mwa wanafunzi na kuwaheshimu walimu, walezi na jumuiya nzima ya shule na jamii inayoizunguka shule.
3. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa masomo na nyakati zingine utakapohitajika kufanya hivyo.
4. Ruhusa zote za kutoka nje ya mipaka ya shule zitatolewa na Ofisi ya malezi au mwalimu wa zamu.
5. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini maalum kutoka katika Ofisi ya malezi na nidhamu.
6. Ni marufuku mwanafunzi kuwatembelea wanafunzi wa jinsia tofauti na yeye wakati wakiwa kwenye mabweni yao.
7. Wanafunzi wote wanapaswa kuishi kama ndugu au kama kaka na dada kwa hiyo ni kosa mwanafunzi kuonesha kwa namna yeyote ile kuwa wanaishi kama mtu na mpenzi wake.
8. Mgeni atakayekutembelea sharti apate kibali kutoka katika uongozi wa shule. Ni marufuku kumtembeza mgeni yeyote katika maeneo ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.
9. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuwa na nywele zisizopunguzwa na kutunzwa vizuri, kunyoa kipara, kufuga ndevu na sharafa, kuacha kucha ndefu na kuvaa mavazi kama vile koti, jaketi, sketi fupi/ iliyofupishwa, kupaka kucha rangi, kutinda nyusi, rasta, lipstick/shine na mapambo yasiyoruhusiwa.
10. Ni marufuku mwanafunzi kuchora au kuandika kwenye kuta, meza, madawati, viti vya kukalia, milango au sehemu nyingine yeyote ambayo hairuhusiwi.

**MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi wa aina yeyote.
2. Uvutaji wa bangi, sigara na madawa ya kulevya.
3. Kupigana, kupiga au kuchochea ugomvi.
4. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi.
5. Kudharau bendera ya taifa na wimbo wa taifa.
6. Kuoa au kuolewa.
7. Kumpa msichana mimba au kupewa mimba au kusaidia kutoa mimba.
8. Kuwa mtoro wa vipindi vya darasani.
9. Kuonekana kwenye nyumba za starehe na kumbi za starehe mfano nyumba ya kulala wageni.
10. Kuwa na simu ya mkononi/line.
11. Kuwa na pasi ya umeme, jiko na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha ajali ya moto.

Kama una tatizo lolote, mawasiliano yafanyike kupitia Uongozi wa wanafunzi, mwalimu wa zamu, walimu wa madarasa na Uongozi wa shule ili kuepusha migogoro shuleni.

Mimi……………………………………………………………….. . nakubali kutii sheria na maagizo haya ya shule.

Pindi nitakapovunja sheria na maagizo haya, hatua kali zichukuliwe kulingana na sheria na taratibu za shule.

Jina na sahihi ya mzazi au mlezi………………………………………………………….. Tarehe…………………………..

APPENDIX: B

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KISIMIRI SECONDARY SCHOOL

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

From the Headmaster,
Kisimiri Secondary School
P.O. BOX 14480
**ARUSHA**

To the Medical Officer

Name of Student …………………………………………………………………………………… (Full name)
Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (1- 4).

1. a. Hearing b. Speech c. Limbs d. Eyesight e. Leprosy f. Epilepsy and g. General diseases
2. Neurosis
3. Pregnancy and
4. Other serious diseases e.g T.B etc

**MEDICAL CERTIFICATION**

a. Hearing……………………………………………………………………………………………….
b. Speech……………………………………………………………………………………………….
c. Limbs ……………………………………………………………………………………………...
d. Eyesight ……………………………………………………………………………………......
e. Leprosy………………………………………………………………………………………………
f. Epilepsy …………………………………………………………………………………………..
g. Other diseases e.g T.B
…...…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………...
……………………………………………..…………………………………………………………

Comment………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………….
Name…………………………………………Signature………………………Date………………………………
Station……………………………………………………..Designation………………………………………

**KIAMBATISHO C:**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI KISIMIRI**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili la mwanafunzi (Selform/Result Slip)…………………………………………………………...
2. Anuani ya nyumbani S. L. P……………………………… Wilaya…………………………………….
3. Mahali alipozaliwa Kijiji/Mtaa……………………Kata ……………………..Tarafa………………….
4. Mahali unapoishi kwa sasa Kijiji/Mtaa………………Kata……………………Tarafa…………………….
   Wilaya……………………………Mkoa………………………
5. Shule ya sekondari uliyotoka/kumalizia kidato cha nne ..……………………………………………..
6. Dini/Dhehebu lako ……………………………… Kabila……………………………………………….
7. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala ya Shule:

   i. Jina kamili la Baba …………………………………………… Namba ya Simu……………
      Hai/Si hai……………………………Kama hai kazi yake……………………………………
      Anwani S.L.P……………………….. Wilaya…………………………………………………..
   ii. Jina kamili la Mama……………………………………………Namba ya Simu……………
      Hai/Si hai……………………………Kama hai kazi yake……………………………………
      Anwani S.L.P……………………….. Wilaya…………………………………………………..

**Bandika picha za watajwa hapo juu kwenye vijisanduku kama wapo hai**

| BABA MZAZI | MAMA MZAZI | MLEZI |
|---|---|---|
| | | |

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi Mwanafunzi…………………………………………………nakubali kwa dhati nafasi niliyopewa na Taifa langu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Kisimiri na nathibitisha kuwa tarifa nilizotoa ni za kweli.Pia nahidi kufuata sheria zote za shule kama zilivyotolewa na zitakazotolewa na Uongozi wa Shule.

………………………….. ………………………….
Saini ya Mwanafunzi Tarehe

**AHADI YA MZAZI**

Mimi Mzazi wa **………………………………………………**naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa mwanangu na kumsisitizia kufuata taratibu zote za shule kama ilivyoelekezwa na itakavyoelekezwa na Uongozi wa shule ili kumpa mwanangu malezi bora yatakayomwezesha kuwa raia mwema na bora wa Taifa letu.

**………………………..** **…………………………**

Saini ya Mzazi/Mlezi Tarehe